# THE MWALIMU NYERERE FOUNDATION

**"AMANI KATIKA BARA LA AFRIKA"**


**MADA ILIYOTOLEWA**
**NA**
**DR. SALIM AHMED SALIM**


**KATIKA KONGAMANO LA DINI MBALIMBALI KUHUSU AMANI, USHIRIKIANO, MAENDELEO NA MAELEWANO KATIKA JAMII**

UKUMBI WA KARIMJEE,
DAR ES SALAAM
TAREHE 6/8/2003

## "AMANI KATIKA BARA LA AFRIKA"

**MADA ILIYOTOLEWA NA**
**MHESHIMIWA DR. SALIM AHMED SALIM**
**KATIKA KONGAMANO LA DINI MBALIMBALI KUHUSU AMANI USHIRIKIANO, MAENDELEO NA MAELEWANO KATIKA JAMII**
**UKUMBI WA KARIMJEE, DAR ES SALAAM**
**JUMATANO TAREHE 6/8/2003**

**Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mzee Alhaj Ali Hassan Mwinyi**

**Waheshimiwa viongozi mbalimbali wa dini**

**Wageni Waalikwa**

**Mabibi na Mabwana**

Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa waandalizi wa kongamano hili, na hasa kwa Sheikh Daktari Mohamed Rukara, Katibu Mkuu wa Baraza la Waislamu Duniani, kanda ya Afrika Mashariki na kati, kwa kunialika nishiriki katika kogamano hili kwa njia ya kuchangia mada.

Nami najiunga na wenzangu katika kutoa pongezi nyingi kwa wazo na maandalizi haya ya kuitisha kongamano linalowajumuisha viongozi wa dini zote, pamoja na viongozi wa serikali, wabunge, mabalozi, na pia viongozi wa taasisi mbali mbali zisizo za kiserikali, ili kuzungumzia suala la amani. Kwa wengi wetu, hatua hii iliyochukuliwa na viongozi wa dini si ngeni kwao, kwa sababu, kama ilivyobainishwa na watoa mada wa awali, msingi mzima wa dini ni amani – amani ya roho, amani ya nafsi, na amani katika mahusiano kati ya kiumbe mmoja na mwingine. Na toka aumbwe mwanaadamu Mwenyezi Mungu amekuwa akituma mitume yake kusisitiza amani miongoni mwao. Viongozi wetu wa dini wamekuwa wakiendeleza jukumu hilo katika maeneo yao mbalimbali.

Aidha, kukutanishwa kwetu leo hapa kwa mkusanyiko tulio nao ni msisitizo kwamba suala la amani sio suala la kisiasa tuu, kwa maana ya kuhimili madaraka ya dola. Hili ni suala pana zaidi linaloingiliana na roho, nafsi, hisia, na hasa mahusiano yetu katika jamii. Ni dhahiri kuwa hakuna apaswae kuwa msitari wa mbele zaidi katika upana huu, isipokuwa viongozi wetu wa dini. Vivyo hivyo, kuwepo kwa pamoja katika ukumbi huu leo, kwa masheikh, maaskofu, mapdri, na wanazuoni wa madhehebu tofauti ni kielelezo kwamba hili ni suala zito linalohitaji tafakari na maelewano ya pamoja. Kwa hakika, mkusanyiko huu leo, katika bandari hii ya salama, sio tuu utachangia katika kuimarisha na kudumisha amani kati ya viongozi waliopo hapa, bali unatoa matumaini kwa waumini wote na kuthibitisha kuwa hatima yetu hapa duniani ni moja na tunahitaji kuhakikisha mazingira ya amani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti
Ndugu washiriki,

Maulamaa waliozungumza awali wamebainisha kwa kina, msisitizo alioweka Mola wetu Muumba, na maadili ya mitume yake kuhusu suala hili la amani. Nina hakika viongozi wetu wa dini na washiriki wengine mtajazia zaidi upeo huo. Mimi ningependa kuelekeza mchango wangu katika kueleza kwa ufupi hali halisi ya amani ilivyo katika bara letu la Afrika, na

nafasi iliyopo katika kudumisha amani, na nikimalizia kwa kuzingatia hatima yetu sisi kama Watanzania.

Takriban, miaka 30 iliyopita kwa bara letu imekuwa ni kipindi chenye masahibu mengi magumu yaliyotokana na kutetereka kwa amani. Tumeshuhudia mapinduzi mengi ya serikali, vita baina ya nchi na nchi, magomvi ndani ya nchi, maangamizi ya kihalaiki, vurugu na mateso mengi kwa watu wetu. Mamilioni wameuawa; mamilioni nyingi wameumizwa, kuteseka na kutiwa vilema; wengi mno wamehamishwa makazi yao, kufanywa wakimbizi, na kuteketezewa mali zao. Bara letu limepoteza nafasi ya maendeleo, limedhihakiwa na kubezwa. Kwa muda mrefu tumehusishwa na mikasa, magomvi, na mambo ya kinyama.

Wakati huu tunavyokutana hapa, wananchi wa Liberia wanaendelea kuuawa na maiti zao zimetelekezwa nje kwa kushindwa kuzikwa. Raia hawana chakula, hawana maji na hawana pa kukimbilia. Wamekuwa hivyo kwa miezi kadhaa na kwa karibu miaka mitano sasa hawajafaidi amani ya kudumu. Huko Burundi, makombora yanaendelea kuunguruma; yakiua na kujeruhi wananchi wasio na hatia. Maisha yamepoteza uhakika na matumaini. Hali imekuwa hivyo karibu miaka kumi sasa. Huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, mamilioni ya wananchi wamepoteza maisha, zaidi ya hapo wameathirika vibaya kwa majeraha, kuhama maskani, na kufanywa wakimbizi. Vita vilivyodumu huko na kuitwa Vita vya Afrika vya Tatu vya Dunia vimezuia utajiri mkubwa wa Kongo usiendeleze wananchi wake na kulinufaisha bara hili. Mateso waliyopata wenzetu huko hayasemeki.

Naweza kutumia muda mrefu sana kueleza hali kama hiyo Somalia, Sudan, Afrika ya Kati na huko kaskazini mwa Uganda ambako wananchi wanateswa na hata watoto kuporwa na kufanyiwa ukatili usiomithilika. Mimi binafsi kamwe sitasahau kumuona huko Sierra Leone miaka michache iliyopita, binti anaeitwa Maimuna, ambae alikatwa mikono yake yote miwili kwa panga, akiwa na umri wa miezi mitatu tuu. Hadi leo binti huyo ameachwa na kilema cha maisha yake yote. Eti, hao waliomkata wanajidai kwamba wamefanya hivyo kwa maslahi ya wananchi wa Sierra Leone. Hadi sasa sijayafahamu maslahi ya aina hiyo yanayohitaji mateso kwa viumbe wachanga wasio na dosari.

Nchini Rwanda tunakumbuka mauaji ya kihalaiki ya zaidi ya Wanyarwanda milioni moja mwaka 1994. Vita vikali vilivyozuka mwaka 1998 baina ya Ethiopia na Eriterea – nchi mbili ambazo zilikuwa na udugu

na uelewano mkubwa – zilisababisha maafa makubwa kwa nchi hizo pamoja na kuuwawa kwa zaidi ya askari laki moja (100,000). Pia tunakumbuka mateso yaliyowapata wananchi wa Côte d'Ivoire hivi karibuni baada ya kutokea migogoro na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Mbali ya madhara ya ndani ya nchi ambapo jamii za makabila ama vikundi mbalimbali vinapigana vyenyewe kwa vyenyewe, nchi za jirani nazo huathirika kutokana na wimbi kubwa la wakimbizi. Kati ya wakimbizi milioni 20 walioko duniani sasa, wakimbizi zaidi ya milioni 4 wako barani Afrika. Tanzania peke yake imekuwa ikipokea na kuhudumia jumla ya mamilioni ya wakimbizi tangu mwaka 1964. Ni moja kati ya nchi chache sana katika Bara hili yenye sifa ya kupokea na kuhifadhi wakimbizi wengi.

Ni muhimu kutambua kwamba licha ya wale wanalazimika kukimbia nchi zao kwa ajili ya kuteswa au kwa hofu ya kuteswa, na kupata hifadhi katika nchi za jirani au kwingineko, kuna kundi kubwa zaidi la watu ambao hawaitwi wakimbizi lakini pia mazingira yao yanafanana na ya wakimbizi. Hawa ni wale wanaolazimika kuyahama majumba yao na maeneo yao na kuishi sehemu nyingine mbali mbali katika makambi kama wakimbizi. Kundi hili ambalo kwa Kiingereza huitwa *Internally displace persons* au IDP, linazidi watu millioni 10 katika bara hili. Mahitaji yao na matatizo yao hayatofautiani sana na ya wakimbizi wa kawaida.

Wapendwa washiriki,

Ni nini hasa kiini cha kuvurugika kwa amani kunakotuletea athari mbaya zinazotuangamiza, kututesa na kutunyima nafasi ya kufaidia baraka alizotupa Mola wetu katika bara hili. Ningependa kugusia maeneo matatu yenye kuambatana na yanayolihusu suala hili.

Kwanza, ni hali inayojengeka katika jamii ya sehemu moja au zaidi ya moja kujiona kuwa wanatengwa na kuhisi kuwa hawamo katika mustakabal wa jamii yao na wala kufaidika katika tija na maendeleo yake. Imetokea mara nyingi, pale ambapo maendeleo ya nchi hayaendi sambamba na maslahi ya wote na kutoa nafasi sawa kwa kila mmoja kuchangia na kuboresha maisha yake. Hiyo hali inajenga uhasama na kama haitadhibitika na kurekebishwa, inaharibu amani. Wahusika wanaweza kuwa ni tabaka, kabila, watu wa eneo maalum, rangi au imani. Utengano wa aina hii unaweza kuwa chocheo la kuvuruga amani ya jamii.

Ni ukweli ulio dhahiri kwamba katika miaka 30 iliyopita katika bara letu zimekuwepo nchi ambazo mifumo ya uendeshaji serikali zake, umilikaji na pia uzalishaji mali, na hata usambazwaji wa huduma za jamii umebagua baadhi ya wananchi wake na kusababisha manun'guniko na uhasama uliovuruga amani. Lakini wakati huo huo imekuwepo hali ya watu wachache wenye uchu wa madaraka kutumia tofauti za imani – ama za ukabila, asili, dini au rangi – na kuzijengea hisia za uhasama na mporomoko wa jamii. Naamini sihitaji kusisitiza kwamba uadui wowote unaojengwa kwa misingi kama hii – yaani dini au kabila au rangi au asili – inakita ndani ya jamii na kuilipua vibaya kwa sababu inatapakaa katika mahusiano ya mtu mmoja na mwingine.

Lakini kama tuonavyo hapa, dini tofauti zinaweza kuwa pamoja na zikazungumza kwa amani na utulivu pamoja na tofauti za misingi ya imani zao. Vivyo hivyo, makabila mbali mbali yanaweza kuishi kwa amani na utulivu kwa karne nyingi na hata kujengea mila za utani baina yao. Aidha, miongoni mwa watu, hakuna tofauti aliyotuumbia Mwenyezi Mungu inayopasa kuwa chanzo cha mfarakano. Tumeambiwa katika misahafu kuwa Mola wetu ametuumba na tofauti ili tutambuane na sio tugombane. Ni bahati mbaya, wapo viongozi katika jamii wametumia tofauti hizi katika bara letu kuleta maangamizo, husda, na mifarakano iliyoleta athari kubwa na inayohitaji muda mrefu sana kuirekebisha.

Hali ya pili iliyochangia mvurugiko wa amani katika bara letu ni kupotoka kwa misingi bora ya uongozi na demokrasia. Siku hizi imejengeka dhana ya utawala bora, ikimaanisha mfumo unaoendeshwa kufuatana na taratibu za kisheria, uwazi, usawa, ufanisi na kuheshimu haki za kibinadamu. Utawala bora unasimama katika mhimili wa demokrasia wa kufuata matashi ya wengi lakini kuzingatia maslahi ya wachache. Kwa muda mrefu hapa kwetu Afrika misingi hii ilivunjwa bila kujali lolote na wananchi walio wengi wakapuuzwa na kukandamizwa ili kukidhi malengo binafsi na kushamirisha rushwa, wizi na upendeleo.

Mara nyingi mifumo ya kupata uongozi halali ilivurugwa na wachache kujitwalia madaraka bila ya ridhaa ya wengi. Chaguzi zilifanywa kuwa ni kiini macho na sera za maendeleo zilipelekwa kihadaa. Haki za binadamu zilivurundwa na wengi kupoteza maisha na mali zao. Hali hii

ilivuruga amani na ikasababisha mtafaruku kati ya wanaotharika vibaya na wale wanaofaidika na ubadhirifu uliopo.

La tatu lililoathiri amani na utulivu katika bara letu ni udhaifu wa taasisi zetu za kisiasa, na pengine kushindwa kwa taasisi zetu za jamii kwa ujumla, kudhibiti mfarakano. Na pengine hapa nitaje tuu kuwa mahala kwingine hata taasisi za dini zilijikuta katika lindi hili.

Maendeleo ya taasisi za jamii nyingine, hasa za magharibi, zimeonyesha kwamba vyombo kama katiba, mahakama, wasajili mbali mbali vinaweza kukuzwa na kuweka mizani ya kuepusha shari na uhasama katika jamii. Ilitokea wakati fulani, huko Marekani kulizuka tofauti kati ya serikali na upinzani katika bunge na kuzuia shughuli za serikali zisifanyike kwa karibu siku 21. Lakini waliweza kumaliza tofauti zao kwa amani na utulivu bila athari kubwa kwa maisha ya watu au utulivu wa jamii.

Vivyo hivyo, viongozi wa dini, wazee kwa ujumla, vyombo vya kitaalam, taasisi zisizo za serikali na vyombo vingi kama hivyo, vina jukumu hapa duniani, pamoja na kazi nyingine, la kuhakikisha kwamba tofauti zozote zilizopo au zinazozuka hazipaswi kufikia hali ya kuleta uhasama na mfarakano. Vyombo hivi vikikosa uwezo wa kutimiza jukumu hili, basi jamii huharibikiwa na kila tofauti ndogo hukua na kuwa uhasama mkubwa. Bara letu lilijikuta katika hali hiyo ambayo ikapelekea kujenga utamaduni wa kwamba kila anaetofautiana nawe ni adui na unapaswa kumuangamiza. Taratibu za siasa zikawa anaepata apate na anaekosa ajijutie. Na inapowezekana ikawa mbinu ifaayo ni kuhakikisha kuwa ukipata basi wengine wasipate na wala wasihusishwe. Hali hiyo ikawa sio tuu katika uongozi wa serikali, bali hata katika mahusiano ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,
Wapendwa washiriki

Pamoja na kuwepo kwa hali ya mtafaruku na Waafrika kuendelea kupoteza maisha kutokana na kuvurugika kwa amani, hatua nyingi zimechukuliwa katika ngazi ya Afrika kwa ujumla, jumuia mbali mbali zilizomo humu barani, nchi za kijirani, na hata nchi moja moja katika kurejesha amani, usalama na utulivu. Umoja wetu wa Nchi Huru za Afrika ambao sasa umejengeka na kuwa Umoja wa Afrika tokea 1993 uliunda chombo cha kuzuia, kudhibiti na kusuluhisha migogoro ambacho sasa kimepewa uwezo mkubwa zaidi na kuwa Baraza la Amani na Usalama. Tokea asili yake, chombo hicho kimejitahidi kukabiliana na migogoro mingi

na kufanikiwa kwa viwango tofauti. Kubwa zaidi ni mafanikio ya kulifanya suala zima la kudumisha amani kuwa ni jukumu la Afrika yote na sio la nchi moja au lenye kukingwa na kipengere cha zamani cha kusema kuwa ni suala la ndani ya nchi na haliingiliwi. Kwa muda wa miaka kumi iliyopita, chombo hiki kimefanya kazi na Umoja wa Mataifa, taasisi mbalimbali za kimataifa, na pia mashirika ya jamii, pamoja na ya kidini katika kukabiliana na migogoro.

Vivyo hivyo, jumuiya kama SADC, ECOWAS, ECCAS, IGAD ambazo ni taasisi za pamoja za maeneo mbali mbali ya bara letu zimekuwa zikijenga uwezo wa kukabiliana na hali ya migogoro. Hivi leo tuu, askari walioandaliwa na ECOWAS wameendelea kumiminika Liberia kuzuia hali mbaya iliyodumu huko kwa muda mrefu. Vile vile viongozi wetu wa SADC pamoja na wenzao wamekuwa msitari wa mbele katika kushughulikia tatizo la Burundi. IGAD nao wamekuwa Kenya muda mrefu kusuluhisha tatizo la Sudan na Somali. Hizi ni hatua za kutia moyo, hasa kwa sababu jumuia hizi za nchi jirani ziko karibu zaidi na matatizo na zina nafasi nzuri sana za kuyakabili.

Pamoja na yote hayo, viongozi wa dini na waumini kwa ujumla tuna nafasi kubwa sana katika kurejesha na kudumisha amani katika bara letu. Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi amefafanua kwa kirefu asubuhi hii mchango wa dini katika kudumisha amani. Mimi ningependa kusisitiza zaidi kuwa nafasi yenu viongozi ni muhimu sana katika kuleta amani na kuidumisha amani hiyo. Kwa sababu mitafaruku inahusisha imani na nafsi za waumini na kwa vile ninyi mumo katika nafasi nzuri zaidi ya kuelekeza imani zetu, basi mna jukumu kubwa sana katika mafundisho, mahubiri na miongozo yenu kudumisha amani. Ama mmesikia au mmeshiriki katika hatua mbalimbali za viongozi wa dini kurejesha amani pale inapotetereka. Kamwe isiwe viongozi ndio mashabiki wa kwanza wa kuchochea uhasama miongoni mwa viumbe wake Mwenyezi Mungu.

Ni wajibu wa viongozi wa dini mbalimbali, pamoja na kukuza imani kwa waumini, pia kuimarisha amani ndani ya jamii kwa kusisitiza maadili mema, mshikamano, ushirikiano wa mawazo na vitendo, njia za kukabiliana na dhuluma ndani ya jamii, ulinzi na utetezi wa haki za wanyonge, usimamizi wa mfumo mzuri wa demokrasia shirikishi na utawala bora. Sote tuna imani kubwa kwamba kutokana na imani waliyonayo jamii kwa viongozi wa dini kama watu safi mbele ya Mwenyezi Mungu, kuhubiri na kusimamia nguzo za utawala bora na demokrasia

ndani ya jamii kwa kuleta amani na utulivu, kutaleta maendeleo ya kudumu katika jamii ya Waafrika.

Pamoja na matatizo yanayotukabili, kwa ujumla nchi yetu Tanzania ni moja ya nchi chache katika bara la Afrika iliyobahatika kuwa na amani na utulivu. Hali hii tulio nayo inatokana na misingi madhubuti iliyojengwa na kuimarishwa na waasisi wa taifa letu na kuendelezwa na viongozi wetu waliopo katika maeneo mbalimbali. Ni muhimu kuienzi na kuiendeleza misingi hii. Tusiidharau na kuifanyia mzaha na wala tusijisahau na kujigamba kwamba hata tukiyapuuza maadili na misingi hiyo hatutadhurika. Viongozi wetu wa dini wana majukumu makubwa katika kuendeleza na kusambaza maadili mema katika kuimarisha utawala bora na demokrasia ili kuweka mazingira mazuri ya kuiletea jamii yetu maendeleo.

Ningependa kusisitiza kuwa amani ikidumishwa katika nchi yeyote ya Afrika itasaidia katika vuguvugu la bara letu katika kuleta maendeleo kwa Waafrika. Katika upeo huo, ni jambo lililo wazi kwamba hali ya amani na utulivu iliyopo katika nchi yetu ni mchango muhimu katika juhudi za bara letu kurejesha na kudumisha amani na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo. Ni tegemeo langu kwamba tunapoendelea na mjadala huu tutakapotoka kwenda kwenye jamii zetu, tunapozungumza na kuhubiri imani kwa jamii zetu, lengo moja liwe kudumisha na kuimarisha maelewano, amani na utulivu kwanza katika jamii, ili shughuli za maendeleo endelevu ziweze kufanikiwa.

Mwisho, ni vyema tukumbushane kwamba amani sio tu kutokuwa na migogoro au vita vya wenyewe kwa wenyewe. Ili kufanikisha amani ya kudumu katika bara letu ni muhimu sana kupambana na yale mambo yanayowakera watu wetu na ambayo ni rahisi kuwa vichocheo vya kuvunjika kwa hali ya amani na utulivu. Kwa hiyo basi, licha ya kuzidisha juhudi zetu ili kumaliza vita vya wenyewe kwa wenyewe katika baadhi ya nchi zetu au magomvi baina ya nchi na nchi, ni jambo la maana na la msingi tupambane na dhuluma, unyanyasaji, uonevu, ukiukwaji wa haki za binadamu, ubaguzi wa aina yoyote ile katika nchi zetu na jamii zetu na kuimarisha misingi ya uelewano, upendo na mshikamano chini ya mifumo ya demokrasia shirikishi na utawala bora. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeandaa na kuimarisha misingi madhubuti ya kurejesha, kulinda na kudumisha amani katika bara letu la Afrika. Katika kufanikisha haya, kila mmoja wetu analo jukumu lake. Tukumbuke wosia wa Baba wa Taifa letu,

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere – "Inaweza kutendeka; kila mmoja atimize wajibu wake."

Ahsanteni!